# Tuwekeze zaidi kupata tija kubwa sekta ya uvuvi



Uvuvi ni miongoni mwa shughuli muhimu za kiuchumi hapa nchini inayochangia kutoa ajira na ukuaji wa pato la taifa. Taarifa za tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi zinaonyesha kwa mwaka 2020/2021 uvuvi ulichangia asilimia 1.8 ya Pato la Taifa pamoja na ajira za moja kwa moja 194,804.

Inakadiriwa pia kuwa Watanzania milioni 4.5 wanaendesha shughuli zao za kiuchumi katika mnyororo wa sekta ya uvuvi kama kushona nyavu, kuchonga boti na biashara ya samaki.

Hata hivyo, tukitizama sekta hii kwa uzoefu wa mazingira bado inakabiliwa na changamoto ambazo kwa mtazamo wetu zinapunguza kasi ya ukuaji wake tukilinganisha na mataifa mengine yaliyoendelea katika sekta hiyo;

Uvuvi wetu bado ni mdogo kwa mtindo na muundo wake, unafanyika kwa zana za kawaida, matumizi ya vyombo kama madau, ngalawa, nyavu, mitumbwi na mengine haitoi ufanisi wa kiushindani na kibiashara;

Kwanza, zana hizo si rahisi kufanya uzalishaji mkubwa ukilinganisha kwa mfano na matumizi ya manowari za uvuvi unaofanyika katika nchi zilizoendelea katika sekta hiyo, mathalani Japan, Indonesia au nchi za ukanda wa Scandinavia.

Taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Annual fisheries statistics report, 2019), inaonyesha jumla ya tani za samaki 470,309.23 zilivuliwa kwa mwaka 2019. Mwaka 2010, Norway imezalisha tani milioni 2.7 za samaki (FAO, fisheries and aquaculture country profile), ambayo ni mara 5 zaidi yetu.

Pili, pia uvuvi huo hauwezeshi kupata mazao ya kutosha kufaidika na fursa za soko, mfano kiukanda na kimataifa, hivyo sekta hiyo inakosa kupata faida kubwa kibiashara kama zinazopatikana, mfano katika kilimo cha ardhini.

Tatu, uvuvi wetu pia hautaweza kutumia kikamilifu fursa ya soko la ndani, ongezeko la idadi ya watu na shughuli kwa mfano za kitalii inaongeza mahitaji ya vyakula bahari, kama uzalishaji haukui kwa kasi inayowiana, fursa ya soko mathalani katika mahoteli ya kitalii ambayo ni watumiaji wazuri wa mazao bahari inaweza kuchukuliwa na makampuni ya nje, na wakaagiza kutoka huko.



**TUJADILIANE**
Rashid Aziz

Upande mwingine, sekta yetu ya uvuvi inahitaji kuongezewa thamani, mathalani kuwekeza katika viwanda vya kuhifadhi na usindikaji samaki, kuchakata vyakula bahari na viwanda vinavyoweza kubuni bidhaa zinazotokana na mazao bahari mbalimbali.

Uvuvi wetu ni kama bado upo katika dhana ya uchuuzi, kinachovuliwa leo kitumike leoleo, ikiwa ni samaki, pweza, ngisi na mengine hawezi kusubiri mpaka kesho ataoza na kuharibika kutokana na kukosekana uwezo wa kuhifadhi. Kukosa uhifadhi katika mnyororo wa uzalishaji maana yake hali ikicheza kidogo, hakuna uhakika wa kuipata bidhaa hiyo sokoni, mazoea haya yanaidumaza sekta hii.

Pia ya Serikali na wadau wa sekta hii kuendeleza jitihada za kutoa mafunzo ya mbinu bora za uvuvi, ili hata ambao bado wanaendeleza vitendo vya uvuvi haramu waelewe na kuacha kabisa.

Mafunzo hayo yatolewe kuhusu kuhifadhi mazalia ya samaki, kuepuka uharibifu wa ekolojia ya bahari na mengine. Hatuwezi kuwa na sekta kubwa na endelevu kwa kuharibu mazingira na mazalio viumbe bahari, kesho tutapata wapi samaki wengine? Tusipokuwa makini mabadiliko ya tabianchi miaka ya mbeleni yanaweza kutuadhibu.

**Wasiliana nami kwa namba 0678745333 au binazizrashid@gmail.com**

# Uvuvi haramu, tozo na mabadiliko ya soko vyavuruga uchumi wa samaki Kanda ya Ziwa

Saada Amir na Anania Kajuni, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz



Baadhi ya wavuvi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wametaja uvuvi haramu, mrundikano wa tozo na matumizi ya taa za betri kuwa ni chanzo cha upungufu wa samaki unaosababisha mauzo yake kushuka ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Tanzania (BoT) iangaziayo ufanisi wa uchumi wa kanda iliyotolewa Oktoba 5 mwaka huu, licha ya uuzaji wa samaki Kanda ya Ziwa kuongoza nchini, lakini umepungua ikilinganishwa na miaka minne iliyopita.

Ripoti hiyo inaonyesha mauzo ya samaki kwa ujumla nchini yameongezeka kufikia tani 94,544.8 mwaka 2022/2023 ikichangiwa na ongezeko la kanda ya Kusini Mashariki, lakini kanda ya ziwa yamepungua kutoka tani 34,863.9 mwaka 2019/20 kufikia tani 27,548.6 mwaka 2022/23.

Mapato yatokanayo na mauzo ya samaki mwaka 2022/2023 yalifikia Sh506.8 bilioni, yakipungua kutoka Sh526.5 bilioni mwaka 2021/2022, lakini yakiongezeka kutoka Sh393.2 bilioni ikilinganishwa na mwaka 2019/2020.

Katibu wa Chama cha Wavuvi Tanzania (Tafu), Jephta Machandalo anasema pamoja na kuwepo uvuvi haramu unaochangia samaki kupungua, kuna uvuvi haramu ambao umehalalishwa na sheria akitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuchukua hatua.

"Samaki wamepungua Ziwa Victoria sababu ya uvuvi haramu unaoendelea, lakini kuna uvuvi ambao umehalalishwa kisheria ambao ni uvuvi wa dagaa.

"Uvuvi wa dagaa umegeuka kuwa uvuvi haramu kutokana na kwamba wavu wa dagaa ni mkubwa sana hauna mipaka, sheria haitamki kwamba wavu wa dagaa unapaswa kuwa na urefu wala upana kiasi," anasema Machandalo na kuongeza:

"Wakati huohuo kuna aina ya nyavu zinazotumika sasa hivi, zile za Japan ambazo matundu yake ni ya pembe nne badala ya matundu ya pembe sita kama ilivyo nyavu ya kawaida, unakuwa kama kitambaa. Ni kuchuja maji tu lakini kila kitu kinapitiwa ziwani wakati wa uvuvi iwe sangara wa kilo 50, 100, awe wa kawaida, wawe watoto wa sangara au dagaa wenyewe.

"Sasa wavu wa namna hiyo huwezi kutegemea uvuvi endelevu hata kama samaki wanazaana, wao wazaane kwa miujiza gani?"

Mwenyekiti wa Muungano wa Wavuvi nchini (Fuo), Juvenary Matagili yeye anasema taa zinazotumika wakati wa uvuvi ni aina nyingine ya uvuvi haramu, akidai zinachangia kupungua kwa mazao ya samaki.

"Uvuvi haramu ndio unasababisha hayo mambo yote, kwa mfano sasa hivi kuna hizi taa ambazo wavuvi wa dagaa wanazitumia. Asilimia zaidi ya 95 ni uvuvi wa kutumia taa za kienyeji ambazo ni za betri. Serikali inasema watumie mwanga usiozidi wati 10, lakini taa zinazotumika sasa hivi ni zaidi ya wati 20... Serikali inajua kabisa kuna taa za kienyeji lakini haichukui hatua," anasema.

Anashauri ili kuondokana na uvuvi haramu suala la kuangalia shughuli za uvuvi libinafsishwe kwenye kampuni binafsi kwa kuwa hakuna watu zaidi ambao wamejizatiti kwenye kazi hiyo.

"Kuanzia ngazi ya chini hadi za juu wote wanajua, lakini sheria hazifuatwi... Uvuvi haramu kuuzungumzia ni ngumu kwa sababu karibu maofisa wote wa uvuvi waliopo wanapendelea rushwa, labda sasa suala la udhibiti wa uvuvi haramu litekelezwe na kampuni binafsi kwa kuwa Serikali hatuna wa kujitoa kwa hilo,"

> **"Wapo viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama nimeshazungumza nao, tunataka tumalize hili tatizo, hatuwezi kila siku kutoa maelekezo wakati hayatekelezwi."**
> Waziri wa mifugo na uvuvi, Abdallah Ulega

anasema Juvenary.

Kiongozi wa wavuvi mkoani Kigoma, Francis John anasema mauzo yameshuka kutokana na kupungua kwa samaki, akidai Ziwa Tanganyika upungufu unatokana na uvuvi haramu na mabadiliko ya tabianchi.

"Uvuvi haramu huku upo wa aina ya filimayaa (wavuvi wanatumia nyavu zinazodaiwa kuwa na sumu ili wapate samaki na dagaa wengi) unaosababisha samaki kuoza masaa machache baada ya kuvuliwa kutokana na kutumia nyavu zenye sumu. Hilo linasababisha samaki kupungua sana ziwa Tanganyika kwa sababu kila wakienda kuvua likipita saa moja samaki wanakutwa wameoza wote," anasema.

Anaiomba Serikali iangalie aina zote za uvuvi haramu na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika watakaokamatwa wakijihusisha na uvuvi huo, ikiwemo kufikishwa kwenye vyombo vya sheria pamoja na kuchomwa moto nyavu wanazozitumia.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Wavuvi Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, Onesmo Langi anasema Serikali imeshindwa kuchukua hatua madhubuti za kuzuia uvuvi haramu ambao bado upo kwa kiasi kikubwa pamoja na kuzuia wavuvi kuvua kwenye mazalia ya samaki, hali inayosababisha samaki na mauzo kupungua.

"Kingine kilichosababisha hali hiyo ni mabadiliko ya hali ya hewa, zamani kulikuwa na miti ambayo imeota kandokando ya ziwa, lakini saizi hivyo vitu havipo, hivyo unakuta samaki anapotoka kwenye kina kirefu anakuja pembezoni ya ziwa ili azaliane anakutana na mazingira mabaya yaliyoathiriwa na shughuli za binadamu.

"Serikali ilitenga maeneo ya mazalia ya samaki, inapaswa kuyasimamia ikiwa ni pamoja kuyawekea alama ambayo kila mtu atajua kuwa maeneo hayo shughuli za uvuvi hazipaswi kufanyika.

"Kuhusu uvuvi haramu naamini Serikali ikiamua jambo haiwezi kushindwa kwa kurudisha jambo hilo katika Serikali za Mitaa, lakini pia Serikali iunde bodi maalumu kwa ajili ya kusimamia suala la uvuvi."

Naye Mwenyekiti wa Wavuvi Mkoa wa [illegible]ra, Matete Mgongo anaiomba Serikali [illegible] mkazo uvuvi haramu, akitolea mfano kuma inaweza kuzuia na kud[illegible]biti madini yasi[illegible]roshwe kwa [illegible]ii inashindwa [illegible]wekeza nguvu ya kulinda [illegible]wa.

"Ukiangalia [illegible]aka mitano kurudi nyuma tulikuwa tukisomesha watoto wetu kwenye shule binafsi za gharama, lakini sasa wavuvi wengi wamewatoa watoto wao huko, wamerudi kwenye shule za umma sababu kipato chao kimeathiriwa na kukosekana kwa samaki," anasema.



Vilevile anasema uwepo wa tozo nyingi nao unachangia mauzo kuporomoka, kwa kuwa baadhi ya wavuvi ili waweze kujiendesha wanalazimika kutorosha mazao ya samaki nje ya nchi.

### Mabadiliko ya soko na tozo

Mwenyekiti wa Tafu, Bakari Kadabi anasema sababu nyingine ya mauzo kuonekana kushuka kulinganisha na miaka ya nyuma ni wavuvi kuamua kuuza mazao yao ya samaki kwenye masoko ya ndani, akidai wanakwepa kuuza viwandani kulingana na malipo kuwa chini, hivyo kusababisha Serikali isipate takwimu sahihi za mauzo ya kitoweo hicho.

"Kuongezeka kwa masoko ya ndani ambayo yanapokea samaki kwa wingi badala ya viwandani. Hii inatokana na bei halisi ya viwandani haiendani na uendeshaji kazi wa wavuvi, kwa hiyo wavuvi wanaona kuliko kuuza kwa kilo moja hadi nne kuanzia Sh11,000 na bora wapasue samaki zao watoe mabondo, wauze mabondo alafu wauze minofu ambapo wanapata faida na kuendelea kukidhi uendeshaji wa kazi zao," anasema.

Machandalo anasema tozo ni sababu nyingine iliyopelekea uuzwaji wa samaki kushuka, akidai wavuvi wanatozwa tozo nyingi zaidi ya 13, hali inayowalazimu baadhi yao kutorosha samaki nchi jirani.

"Yaani samaki mmoja sangara anaweza kuwa na zaidi ya tozo 13 na bado zimeongezwa tozo nyingine. Sasa uendeshaji unakuwa ni mgumu, matokeo yake tuna samaki wengi wanatoroshwa. Samaki wenyewe ni haba, lakini na wale wanaopatikana kidogo wanatoroshwa juu kwa juu," anasema.

Mtafiti wa uvuvi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania mkoani Mwanza (Tafiri), Philemon Nsinda anasema matumizi ya zana haramu, mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la uvuvi haramu ni sababu ya samaki kupungua na kusababisha mauzo ya kitoweo hicho kushuka.

### Hatua za kudhibiti

Kufuatia kuendelea kwa vitendo vya uvuvi haramu, Novemba 28, 2023 Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alimuagiza Mkurugenzi wa Uvuvi, Profesa Mohamed Sheikh kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha ndani ya mwezi mmoja wanakomesha.

"Wapo viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama nimeshazungumza navyo, tunataka tumalize hili tatizo, hatuwezi kila siku kutoa maelekezo wakati hayatekelezwi," alisema.

Akizungumza na *Mwananchi* kwa simu kuhusu mikakati ya kuzuia uvuvi haramu, aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa uvuvi, Stephen Lukanga alisema Serikali inafanyia kazi suala hilo, huku akidai wizara hiyo ina mpango wa kuanzisha mamlaka itakayodhibiti suala hilo.

"Kuna mikakati fulani tumeweka ambayo hatuwezi kuiweka wazi kwa sababu hizi ni kazi za kiintelijensia ambazo baada ya kufanya uchunguzi na kubaini maeneo na watu wote wanaohusika na uvuvi haramu tutaweka wazi," alisema Lukanga, aliyekuwa akikaimu nafasi hiyo hadi Oktoba mwishoni.

Aliongeza: "Mpango mkakati wa muda mrefu wizara inajipanga kuanzisha mamlaka, tumeona mbinu nyingi zikitumika huwa hazizai matunda, unadhibiti leo uvuvi haramu halafu kesho unarudi tena, hivyo tunataka tufanye kama wenzetu wa Maliasili na Utalii, wameanzisha kupambana na ujangili".

**FAHAMU>**

## Hali ya mauzo ya samaki aina ya sangara ndani ya miaka minne.

**Taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2022 iliyotolewa na Wizara ya Fedha za Mipango inaonyesha mauzo ya samaki aina ya sangara nje ya nchi yamepungua, huku matumizi ya ndani ya kitoweo hicho yakiongezeka.**

**Taarifa hiyo inaonyesha mauzo yamepungua kwa zaidi ya asilimia 30. Mwaka 2019 ziliuzwa tani 32,609 zenye thamani ya Sh400.2 bilioni, wakati mwaka 2020 ziliuzwa tani 24,173 zenye thamani Sh302.3 bilioni.**

**Kwa mwaka 2021 taarifa inaonyesha ziliuzwa tani 21,846 zenye thamani ya Sh337.3 bilioni, huku mwaka 2022 ziliuzwa tani 21,647 sawa na Sh375.4 bilioni.**

**Taarifa hiyo inaonyesha mauzo hayo ya sangara kwa miaka minne nje ya nchi yaliingiza Serikali Sh49.9 bilioni kama mapato yatokanayo na ushuru.**

**Hata hivyo, takwimu za mauzo ya sangara nje ya nchi zimekuwa zikipanda na kushuka katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, kiwango cha juu cha mauzo nje ya nchi katika muongo uliopita ni mwaka 2013 ambapo ziliuzwa tani 33,733.**

# Wanawake wafugaji waibuka kidedea kimataifa

**Na MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo amekabidhi tuzo ya Wanawake katika Uongozi kwa Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC) Tanzania baada ya kuibuka mshindi wa kwanza kati ya washindani 500 kutoka nchi mbalimbali duniani.

Tuzo hiyo imetolewa na Taasisi ya Global Centre on Adaptation (GCA) jijini Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu ambako unafanyika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28).

Akikabidhi tuzo hiyo kwa Kiongozi wa Baraza hilo kutoka jamii ya wafugaji, Maanda Ngoitiko aliyeipokea kwa niaba ya baraza hilo, Dk. Jafo aliwapongeza kwa kuipatia Tanzania sifa.

"PWC wameiheshimisha Tanzania na kuifanya isikike duniani na nina uhakika kabisa tuzo hii imetokana na juhudi binafsi za dada yangu Maanda za kuimarisha uwezo wa uongozi wa wanawake wafugaji kwa kuwajengea uwezo kiasi cha kufikia usawa katika kutoa uamuzi katika jamii zao," alisema.

Akishukuru kwa tuzo hiyo, Maanda alisema kuwa baraza hilo linawahudumia wanawake na wasichana kutoka jamii za wamasai, sonjo, akie na barabaig.

Aliongeza kuwa PWC ni shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi Kaskazini mwa Tanzania kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo ya jamii kupitia uwezeshaji wa wanawake na wasichana wa Kimasai.

Wakati huo huo Tanzania inaendelea kushiriki mkutano wa COP 28 sanjari na mikutano ya pembezoni, mikutano ya uwili na warsha, ambapo watu zaidi ya 81,000 kutoka nchi zaidi 190 wanahudhuria.

Tanzania imeandaa banda la maonyesho katika viwanja vya Dubai Expo City likisheheni wizara na taasisi mbalimbali ambapo ofisi ya makamu wa rais inawakilishwa na Waziri Dk. Jafo, Katibu Mkuu, Mary Maganga na wataalamu mbalimbali.

Mkutano huo unaochagizwa na kaulimbiu ya kitaifa 'Kuimarisha Kilimo Himilivu na Uchumi wa Buluu katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi' ulifunguliwa rasmi Novemba 30, mwaka huu na unatarajiwa kuhitimishwa Desemba 12, mwaka huu.

**BABDA**

## MAONYESHO

Tanzania imeandaa banda la maonyesho katika viwanja vya Dubai Expo City likisheheni wizara na taasisi mbalimbali ambapo ofisi ya makamu wa rais inawakilishwa na...

# SMZ: Mazingira ya uwekezaji mamlaka ya uvuvi yaimarika

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema mazingira ya uwekezaji katika Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DFSA), yameimarika hatua ambayo imewezesha zaidi ya kampuni 100 kupewa leseni za kuendesha shughuli hizo.

Kauli hiyo, ilitolewa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame, alipotoa ufafanuzi kuhusu maendeleo makubwa yaliyofikiwa kwa kampuni za kimataifa kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu.

Makame, alisema katika kipindi cha miaka mitatu, mafanikio makubwa yamefikiwa katika usajili wa meli za uvuvi kupitia mamlaka hiyo yenye makao makuu yake Fumba Zanzibar.

Alisema mafanikio hayo, yanatokana na marekebisho makubwa ya sheria ya mamlaka hiyo iliyofanywa na bunge, ambayo yamefungua uwekezaji zaidi na kuondosha vikwazo vilivyokuwepo awali.

Kwa mujibu wa Makame, wawekezaji wa Kampuni ya Albakora ya Hispania, wanatarajia kujenga kiwanda kikubwa cha kusarifu minofu ya samaki jijini Tanga.

Waziri huyo, alisema wapo wawekezaji kutoka China na Uarabuni, wameonesha nia ya kujenga viwanda vya kusarifu na kuongeza thamani.

"Katika marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, tumewataka wawekezaji kujenga viwanda vya kuzalisha na kuongeza thamani ya bidhaa za samaki, hatua ambayo itawawezesha wavuvi kupiga hatua kubwa ya mapato," alisema.

Alisema serikali zote mbili, zimejipanga

Uhuru Uk. 10, Disemba 7, 2023

CamScanner

# SMZ: Mazingira ya uwekezaji mamlaka ya uvuvi yaimarika

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema mazingira ya uwekezaji katika Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DFSA), yameimarika hatua ambayo imewezesha zaidi ya kampuni 100 kupewa leseni za kuendesha shughuli hizo.

Kauli hiyo, ilitolewa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame, alipotoa ufafanuzi kuhusu maendeleo makubwa yaliyofikiwa kwa kampuni za kimataifa kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu.

Makame, alisema katika kipindi cha miaka mitatu, mafanikio makubwa yamefikiwa katika usajili wa meli za uvuvi kupitia mamlaka hiyo yenye makao makuu yake Fumba Zanzibar.

Alisema mafanikio hayo, yanatokana na marekebisho makubwa ya sheria ya mamlaka hiyo iliyofanywa na bunge, ambayo yamefungua uwekezaji zaidi na kuondosha vikwazo vilivyokuwepo awali.

Kwa mujibu wa Makame, wawekezaji wa Kampuni ya Albakora ya Hispania, wanatarajia kujenga kiwanda kikubwa cha kusarifu minofu ya samaki jijini Tanga.

Waziri huyo, alisema wapo wawekezaji kutoka China na Uarabuni, wameonesha nia ya kujenga viwanda vya kusarifu na kuongeza thamani.

"Katika marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, tumewataka wawekezaji kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha na kuongeza thamani ya bidhaa za samaki, hatua ambayo itawawezesha wavuvi kupiga hatua kubwa ya mapato,"alisema.

Alisema serikali zote mbili, zimejipanga



# UFUGAJI BORA WA SAMAKI

UFUGAJI wa samaki ni shughuli ya kuwaweka na kuwatunza samaki katika bwawa kwa kanuni za ufugaji bora wa samaki ili wapatikane pale watakapohitajika kwa ajili ya chakula au biashara.

**Kanuni za ufugaji bora wa samaki**

1. kuchagua eneo bora linalofaa kuchimba bwawa la samaki
2. kupima na kuchimba bwawa kwa namna sahihi
3. kujaza maji yasiyo na madhara katika bwawa la kufugia
4. kupandikiza samaki kwenye bwawa na kuwatunza vizuri
5. kutunza bwawa lisiharibike kwa mmomonyoko au magugu
6. kuvua samaki bwawani muda wa kufanya hivyo unapowadia
7. kutayarisha na kuhifadhi samaki kwa namna inayofaa
8. kuuza samaki na kutunza kumbukumbu za shughuli zote

**Athari za kutofuata kanuni za ufugaji bora**

**Kuchagua eneo linalofaa**

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kuchimba bwawa mahali ambapo halitadumu, kwa kuingiliwa na mafuriko au kukosa chanzo cha maji ya kujaza bwawa.

**Kupima na kuchimbwa bwawa kwa usahihi**

Matokeo yake ni kuchimba bwawa visivyo na kutofikia kikamilifu kwa lengo la ufugaji samaki

**Kujaza maji yasiyokuwa na madhara:**

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kupata hasara kwa samaki kudhurika na kushindwa kufikia lengo.

**Kupandikiza samaki na kuwatunza**

Kutofuta kanuni hii, matokeo yake ni samaki kudhurika na kufa kwa kukosa matunzo .

**Kutunza bwawa lisiharibike**

Kwenda kinyume na kanuni hii, matokeo yake ni bwawa kubomoka na kuchafuka kutokana na magugu na takataka.

**Kuuza samaki na kutunza kumbukumbu:**

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kupata hasara ya kukosa mapato na kutojua hasara na faida ya shughuli iliyofanyika.

**Vifaa**

a. zana za kufyekea na kuchimbia kama panga, jembe, chepe na toroli
b. zana za kupimia kama kamba, futikamba, mambo na nyundo.
c. Zana za kutengeneza wigo kama nguzo, fito, misumari na waya

Inaendelea Uk 1

CamScanner

# Muswada kudhibiti uvuvi haramu

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema kuwapo kwa Muswada wa kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti, Uvuvi na Maliasili za bahari kwa kiasi kikubwa kutasaidia matumizi bora ya rasilimali za baharini kuwa endelevu na kupambana na uharibifu ikiwemo uvuvi haramu.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame wakati akiwasilisha muswada huo mbele ya wajumbe wa baraza la wawakilishi.

Alisema sera ya uchumi wa buluu imejikita katika kulinda rasilimali za baharini kuona kwamba zinakuwa endelevu pamoja na kuwepo kwa utafiti baharini.

Muswada huo utaunda taasisi ambayo itafanya utafiti katika masuala ya viumbe vya baharini na utajiri wake kwa ujumla.

Makame alisema utafiti unahitajika kufanywa kuona uhai wa viumbe vya baharini ikiwamo matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki baharini.

Alisema matumbawe yamekuwa yakiharibiwa kwa sababu mbalimbali hatua ambayo ni tishio kwa uhai wa viumbe vya baharini kwa sababu ndiyo mazalia ya samaki.

"Taasisi ya utafiti wa viumbe baharini ndiyo tegemeo katika sera ya uchumi wa buluu ambayo itafanya utafiti kujua rasilimali za baharini zikoje kwa mustakabali wa taifa," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia muswada huo wameitaka wizara kufanya utafiti kujua maendeleo ya zao la mwani ambao kwa asilimia 90 hulimwa na wanawake vijijini.

Mwakilishi wa Jimbo la Chambani, Bahati Khamis Kombo (CCM) alisema utafiti unahitajika kwa ajili ya maendeleo ya zao la mwani na kujua hatima yake katika mikakati ya uzalishaji na kufikia viwango vya soko la kimataifa.

"Tunahitaji utafiti ambao utawawezesha wakulima wa kilimo cha mwani kujua hatima yake kufuatilia kuwepo kwa mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili dunia," alisema.

Aidha, Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame Ali (CCM) alisema utafiti unahitajika kwa ajili ya kujua hatima ya kilimo cha mazao ya baharini kutokana na kujitokeza kwa matukio ya uvuvi haramu yanayotishia mustakabali wake.

"Wavuvi wameingia katika wasiwasi mkubwa na hofu kuhusu matumizi mabaya ya uvuvi unaotishia na kuathiri uhai wa viumbe vya baharini kutokana na uvuvi haramu," alisema.